



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MKURANGA



KUMB.Na.MDC/L.20/6/VOLXXXVII/128

20/11/2023

Mkurugenzi,
Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

**YAH: TAARIFA YA UPATIKANAJI PAMOJA NA RAMANI YA UPIMAJI YA KIWANJA
NA. 1 KITALU 'Y' MWANAMBAYA -MKURANGA**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu,

2. Kampuni ya kigeni ya **BU BU GAO FOOTWEAR LIMITED** yenye usajili wa Na.73473.

Kampuni imenunua eneo lenye ukubwa wa ekari 1.2 kutoka kwa **Ndg. Eva -Marry Kitandu** kwa mkataba wa tarehe **15/09/2021**. Mauziano haya yalishuhudiwa na Uongozi wa Serikali ya Kijiji cha Mwanambaya baada malipo ya fidia ya ardhi hiyo kukamilishwa.

3. Baada ya manunuzi hayo, Kampuni iliomba kupanga na kupima eneo hilo kwa matumizi ya kiwanda cha kutengeneza bidhaa za plastic, viatu, samani na bidhaa za mpira ili kuendelea kupanua uwekezaji wao. Mchoro wa Mipango Mji uliandaliwa na kusajiliwa kwa Na. **19/MKR/05/022011** na upimaji kukamilishwa kwa usajili wa Plan Na. **81608**.

4. Hivyo, taratibu za uandaaji wa Hati zinatakiwa kuanza kwa kupata kibali kutoka Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC)

5. Asante kwa ushirikiano wako

Godson Mushi

**KNY: MKURUGENZI MTENDAJI (W),
MKURANGA.**



Nakala :- Kamishna wa Ardhi Msaidizi
Mkoa wa Pwani
S.L.P 9230,
DAR ES SALAAM.

: Mkurugenzi Mtendaji (W)----- Aione kwenye jalada
S.L.P 10
MKURANGA.

Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, S.L.P 10, Mkuranga, Simu: 023-2110038, Nukushi: 023-2110038, Barua pepe: ded@mkurangadc.go.tz, Tovuti: